



NOOR
International



Tafakari zinazoongoza kwenye imani



noor.gallery

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

● Kwa jina la Allah Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu ●

وَأَلْقَى فِي الْأَرْضِ رَوَاسِيَ أَنْ تَمِيدَ بِكُمْ
وَأَنْهَرًا وَسُبُلًا لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٥﴾
وَعَلَّمَتِ بِالنَّجْمِ هُمْ يَهْتَدُونَ ﴿١٦﴾

[النَّحْلِ: ١٥: ١٦]

Na akaweka ardhini milima (majabali) madhubuti ili ituliye (isiiname upande mmoja) isiwamwage, na mito na njia ilimpate kuongoka (njia iliyo sawa) Na (ameweka ardhini) alama, (mnazotumia kujua njia) na kwa nyota wao wanajiongoza

Qurani (16:15-16)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



هُوَ اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ قَرَارًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً
وَصَوَّرَكُمْ فَأَحْسَنَ صُورَكُمْ وَرَزَقَكُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ
ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ فَتَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٤﴾

[غَافِرٍ: ٦٤]

Ni Allah aliye kufanyieni ardhi kuwa ni pahala pa kukaa, na mbingu kuwa dari. Na akakutieni sura, na akazifanya nzuri sura zenu, na akakuruzukuni vitu vizuri. Huyo ndiye Allah Mola wenu Mlezi. Basi ametukuka Allah Mola Mlezi wa walimwengu wote

Qurani (40:64)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



﴿أَلَمْ نَجْعَلِ الْأَرْضَ مِهْدًا ﴿٦﴾ أَلَمْ نَجْعَلِ الْأَرْضَ مِهْدًا
﴿٧﴾ وَخَلَقْنَاكُمْ أَزْوَاجًا ﴿٨﴾ وَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتًا ﴿٩﴾
وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ لِبَاسًا ﴿١٠﴾ وَجَعَلْنَا النَّهَارَ مَعَاشًا ﴿١١﴾﴾

[النَّبَأِ: ٦: ١١]

Je, kwani hatukuifanya ardhi (kama) tandiko? Na milima kuwa (kama) vigingi? Na Tukakuumbeni kwa jozi; (wanaume na wanawake)? Na tukafanya kulala kwenu ni mapumziko? Na tukaufanya usiku (ni kama) nguo (ya kukufunikeneni)? Na tukaufanya mchana ni wa kuchumia [kutafuta] maisha?

Qurani (78: 6-11)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA





هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجْنَا بِهِ نَبَاتَ كُلِّ شَيْءٍ
فَأَخْرَجْنَا مِنْهُ خَضِرًا نُخْرَجُ مِنْهُ حَبًّا مُتَرَاكِبًا وَمِنَ النَّخْلِ مِنَ
طَلْعِهَا قِنْوَانٌ دَانِيَةٌ وَجَنَّاتٍ مِّنْ أَعْنَابٍ وَالزَّيْتُونَ وَالرُّمَّانَ
مُشْتَبِهًا وَغَيْرَ مُتَشَبِهٍ ۗ انظُرُوا إِلَى ثَمَرِهِ إِذَا أَثْمَرَ وَيَنْعِهِ ۗ إِنَّ فِي
ذَٰلِكُمْ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٩٩﴾

[الأنعام: ٩٩]

Na yeye ndiye aliyeteremsha maji (mvua) kutoka mawinguni, basi kwa maji hayo tukatoa (tukaotesha) mimea ya kila kitu (aina). Tumetoa humo mimea ya kijani (ambapo) tunatoa kutokana na hiyo (mimea ya kijani) punje zilizopandana. Na katika mitende katika makole yake yapo yaliyoinama, na bustani za mizabibu na mizaituni na makomamanga yaliyofanana na yasiyofanana. Angalieni matunda yake yanapozaa na yanapoiva. Hakika, katika hayo kuna alama (mazingatio) kwa wanaoamini

Qurani (6:99)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



هُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ
مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَكُمْ وَسَخَّرَ لَكُمُ الْفُلُوكَ
لِتَجْرِيَ فِي الْبَحْرِ بِأَمْرِهِ وَسَخَّرَ لَكُمْ الْأَنْهَارَ ﴿٣٢﴾

[إِبْرَاهِيمَ: ٣٢]

Allah ndiye aliyeziumba mbingu na ardhi, na akateremsha maji kutoka mawinguni. Na kwa hayo akatoa matunda kuwa ni riziki yenu. Na akayatiisha majahazi yanayopita baharini kwa amri yake, na akaitiisha mito ikutumikieni (kwa manufaa yenu mbalimbali)

Qurani (14: 32)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



﴿ ٣٥ ﴾ أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمْ الْخَالِقُونَ ﴿ ٣٦ ﴾
﴿ ٣٦ ﴾ أَمْ خَلَقُوا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بَلْ لَا يُوقِنُونَ ﴿ ٣٦ ﴾

[الطُّور: ٣٥-٣٦]

Au wameumbwa pasipo na kitu chochote (bila ya muumba) au wao ndio waumbaji? Au wameumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini

Qurani (52: 35-36)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA





هَيَّا أَيُّهَا النَّاسُ إِن كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّنَ الْبَعْثِ فَإِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِّن تُّرَابٍ
 ثُمَّ مِّن نُّطْفَةٍ ثُمَّ مِّن عِلْقَةٍ ثُمَّ مِّن مُّضْغَةٍ مُّخَلَّقَةٍ وَغَيْرِ مُخَلَّقَةٍ لِّنُبَيِّنَ لَكُمْ
 وَنُقَرِّ فِي الْأَرْحَامِ مَا نَشَاءُ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ثُمَّ نُخْرِجُكُمْ طِفْلًا ثُمَّ لِتَبْلُغُوا
 أَشُدَّكُمْ وَمِنْكُمْ مَّن يُتَوَفَّىٰ وَمِنْكُمْ مَّن يُرَدُّ إِلَىٰ أَرْذَلِ الْعُمُرِ لِكَيْلَا
 يَعْلَمَ مِّن بَعْدِ عِلْمٍ شَيْئًا وَتَرَى الْأَرْضَ هَامِدَةً فَإِذَا أَنزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ
 اهْتَزَّتْ وَرَبَّتْ وَأَنْبَتَتْ مِن كُلِّ زَوْجٍ بَهِيجٍ ﴿٥﴾

[الحج: ٥]

Enyi watu! Ikiwa nyinyi mna shaka ya kufufuliwa basi kwa hakika Sisi tulikuumbeni kutokana na udongo, kisha kutokana na manii, kisha kutokana na kipande cha damu ilio gandana, kisha kutokana na kipande cha nyama chenye umbo na kisicho kuwa na umbo, ili tukubainishieni. Nasi tunakiweka katika matumbo ya uzazi tunacho kitaka mpaka muda ulio wekwa. Kisha tunakutoeni kwa hali ya mtoto mchanga, kisha mfikie kutimia akili. Na wapo katika nyinyi wanao kufa, na wapo katika nyinyi wanao rudishwa kwenye umri wa unyonge kabisa, hata mtu awe hajui kitu baada ya kuwa anakijua. Na unaiona ardhi imetulia kimya, lakini tunapo yateremsha maji juu yake husisimka na kututumka, na kumea kila namna ya mimea mizuri

Qurani (22: 5)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



هُوَ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَوَاتٍ طِبَاقًا مَّا تَرَى فِي خَلْقِ
الرَّحْمَنِ مِن تَفَوُّتٍ فَأَرْجِعِ الْبَصَرَ هَلْ تَرَى مِن
فُطُورٍ ﴿٣﴾ ثُمَّ أَرْجِعِ الْبَصَرَ كَرَّتَيْنِ يَنقَلِبْ إِلَيْكَ
الْبَصَرُ خَاسِئًا وَهُوَ حَسِيرٌ ﴿٤﴾

[المُلْكِ: ٣-٤]

Ambaye ameumba mbingu saba zilizo tabaka tabaka. Huoni tofauti yoyote katika uumbaji wa Rahmani (Allah Mwingi wa rehema). Basi rudisha macho (uangalie uumbaji wa Allah); Je, unaona kasoro yoyote? Halafu rudisha tena macho mara mbili (ili uhakikishe), macho yako yatakurudia yakiwa yametahayari na kunyong'onyea sana

Qurani (67: 3-4)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



اللَّهُ الَّذِي رَفَعَ السَّمَوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا ثُمَّ
 أَسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلَّ
 يَجْرِى لِأَجَلٍ مُّسَمًّى يُدَبِّرُ الْأَمْرَ يُفَصِّلُ الْآيَاتِ
 لَعَلَّكُمْ بِلِقَاءِ رَبِّكُمْ تُوقِنُونَ ﴿٢﴾
 [الرَّعْدِ: ٢]

Allah (pekee ndiye) aliyeziinua mbingu bila ya
 nguzo mnazoziona. Kisha amelingana sawa juu
 ya Arshi. Na amelitiisha jua na mwezi (kwa
 manufaa na maslahi ya viumbe). Kila kimoja
 (kati ya jua na mwezi) kinakwenda (kwenye
 mhimili wake) kwa muda maalumu. (Yeye Allah
 ndiye) Anayeendesha mambo (yote), anafafanua
 Aya ili mpate kuwa na yakini ya kukutana na
 Mola wenu Mlezi

Qurani (13: 2)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



﴿ ۱۸ ﴾ وَإِلَى الْجِبَالِ كَيْفَ
﴿ ۱۹ ﴾ نُصِبَتْ ﴿ ۲۰ ﴾ وَإِلَى الْأَرْضِ كَيْفَ سُطِحَتْ ﴿ ۲۰ ﴾

[الغاشية: ۱۸-۲۰]

Na mbingu jinsi ilivyo inuliwa? Na milima
jinsi ilivyo thibitishwa (simamishwa)? Na
ardhi jinsi ilivyo tandazwa?

Qurani (88: 18-20)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA





NOOR
International



noor.gallery